

## **SERA YA MIKOPO KWA WANACHAMA WASTAAFU**

### **WA NYUMBA SAVINGS AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LTD**

**REG.NO.1904-DAR ES SALAAM**

#### **UTANGULIZI**

Sera ya Mikopo ni utaratibu unaoandaliwa kuweka ukomo na uwiano wa kukopesha wanachama Wastaafu kwa kuzingatia Masharti ya chama, Sheria ya vyama vya Ushirika Na. 6 ya 2013, kanuni za mwaka 2015 na 2016, nyaraka na Maagizo mbalimbali ya Mrajis wa vyama vya Ushirika.

Sera hii ya mikopo imeandaliwa kwa ajili ya Nyumba SACCOS ili kuweka wazi taratibu za ukopeshaji Wanachama wastaafu .

#### **1. MADHUMUNI YA SERA YA MIKOPO**

- Kuondoa uwezekano wa kufanya maamuzi bila kufuata utaratibu uliokubalika na itakuwa ni mhimili wa kusimamia shughuli zote za Mikopo kwa Wastaafu..
- Kuwapa fursa wanachama wastaafu kuendelea kutumia chama walichokijenga kwa miaka mingi kwa kuboreha maisha yao.

#### **2.0 AINA ZA MIKOPO**

Kutakuwa na aina mbili za mikopo kama ifuatavyo:-

- i. Mikopo ya kuboresha hali ya maisha kama vile afya, elimu, ujenzi wa nyumba, viwanja, ununuzi wa vifaa samani, kilimo matengenezo ya Nyumba na biashara yaani (MIKOPO YA MAENDELEO)
- ii. Mikopo kwa ajili ya dharula.

2.1 Mwanachama mstaafu anaweza kuwa na mikopo ya aina zote mbili bila kuathiri matakwa ya Sera hii.

#### **3.0 ADA ZA MIKOPO (Loan processing fees)**

Mikopo yote itakuwa na gharama za utayarishaji, ili kufidia gharama hizo ada ya 0.5% (ambayo ada ya mkopo ni 0.25% na Mfuko wa Tahadhali 0.25% ) itatozwa kwa kiasi kitakachoombwa na italipwa kabla Mkopo kutolewa.

#### **4.0 UKOMO WA KIWANGO CHA MIKOPO**

Ukomo wa kiwango cha mkopo kwa Wanachama Wastaafu itakuwa kama ifuatavyo:-

- i. Mikopo ya Maendeleo itatolewa mara mbili ya akiba zake alizoweka chamani.
- ii. Mikopo ya Dharula itatolewa si zaidi ya Milioni moja(Tsh 1,000,000/=)

## **5.0 UTARATIBU WA UTOAJI MIKOPO**

5.1 Utaratibu wa utoaji Mikopo kwa Wanachama Wastaafu wa NYUMBA SACCOS LTD hautazidi miezi 36 ili kuweka mzunguko wa fedha vizuri.

5.2 Wanachama Wastaafu pekee waliotimiza wajibu wao ipasavyo kwa NYUMBA SACCOS LTD na walioweza kutosheleza matakwa ya Sera hii watakuwa na haki ya kupokea Mikopo yao.

5.3 Maombi ya Mikopo kwa NYUMBA SACCOS LTD ni lazima yafanyike katika fomu maalum na lazima kila fomu ieleze kiasi cha mkopo kilichoombwa na madhumuni ya mkopo .

5.4 Mikopo ya maendeleo itakuwa inatolewa na Kamati ya Mikopo mara mbili kwa mwezi.

5.5 Mikopo ya Dharura itakuwa inatolewa kila wiki.

## **6.0 UCHANGIAJI WA AKIBA**

6.1 Mwanachama Mstaafu atachangia kiwango cha chini Tsh 25,000/=ya kiwango cha chini cha Mwanachama asiye Mstaafu au kiwango chochote kitakachopangwa na Mkutano Mkuu.

6.2 Uchangiaji huo unaweza lipwa mara moja kwa kipindi chote kwa mwaka au kila mwezi kama wanachama wengine.

## **7.0 KUJADILI/ KUTOLEWA MIKOPO**

- i. Maombi ya mikopo yatajadiliwa katika vikao halali vitakavyofanywa na Kamati ya Mikopo ya NYUMBA SACCOS LTD.
- ii. Maamuzi ya kutoa au kutotoa mkopo yataamuliwa na Kamati ya Mikopo kufuatana na matakwa ya Sera hii.

## **8.0 DHAMANA YA MKOPO**

i.Hisa na Akiba za Wanachama Wastaafu zilizowekwa NYUMBA SACCOS LTD zitachukuliwa kama Dhamana ya Mkopo wa Mwanachama huyo.

ii.Ili mstaafu aweze kupata mkopo atalazimika kudhaminiwa na wadhamini wawil(2) ambao ni ndugu wa familia na mwanachama yeyote wa Nyumba Saccos ltd.

iii.Awe na dhamana isiyohamishika

## **9.0 RIBA YA MIKOPO**

9.1 Mkopo utatozwa riba, riba itatofautiana kulingana na aina ya Mkopo na muda wa urejeshaji.

9.2 Viwango vya faida na riba juu ya Mikopo vitatozwa kila mwezi kwa mtindo wa tozo la salio lililobakia (Reducing Method) kwa kiwango cha Mkopo.

9.3 Riba juu ya Mkopo wa Maendeleo itakuwa 1.0% kwa mwezi na 2.08% kwa mwezi kwa Mikopo ya Dharura.

9.4 Mkopo utalipwa riba kwa kipindi chote ambacho Mkopaji atakuwa amekaa na Mkopo kulingana na salio lililobakia.

9.5 Mkopaji atakayetaka kurejesha Mkopo kabla ya muda wake kumalizika, (kwa mfano Mkopo wa miezi kumi na mbili akalipa ndani ya miezi 6) au kupunguza mkopo kwa asilimia Hamsini (50%) atapata punguzo la 30% salio la riba na punguzo hilo litafanyika mara moja tu.

9.6 Mkopaji atalipa riba yote ya miezi sita kwa Mkopo wa Dharura.

## **10.0 MAREJESHO YA MIKOPO**

10.1 Mikopo ya Maendeleo itarejeshwa kwa kipindi cha miezi 36.

10.2 Mikopo ya Dharura itarejeshwa kwa kipindi cha mwaka mmoja (miezi 12)

10.3 Utaratibu wa marejesho kwa Mikopo yote utakuwa ni malipo ya mwezi ya Mkopo pamoja na riba kulingana na mtiririko maalum wa Marejesho ya kila mwezi ulioidhinishwa tangu siku ambayo Mkopo umetolewa. (Repayment Schedule)

10.4 Iwapo kumetokea ucheleweshaji wa urejeshi mkopo, NYUMBA SACCOS LTD italazimika kuchukua dhamana za Mwanachama Mstaafu kwa kiwango kilichocheleweshwa pamoja na faida yake bila taarifa kwa Mwanachama.

10.5 Mwanachama Mstaafu ataruhusiwa kurejesha kupitia pensheni zake na mapato mengine kutoka kwenye shughuli zake.

Imesainiwa na:

.....

**KATIBU TAREHE MWENYEKITI**